

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA NANE

17 APRILI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA NANE – TAREHE 17 APRILI, 2024

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

93. **MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON
GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Utawala Hospitali ya Wilaya Kasulu.

94. **MHESHIMIWA CHARLES MUGUTA KAJEGE
(MWIBARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya Kisorya, Kasuguti na Kasahunga - Mwibara.

95. MHESHIMIWA BENARDETA KASABAGO MUSHASHU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaajiri Walimu wa kutosha wa Somo la Hisabati na Sayansi ili kuliokoa Taifa letu kukosa Wanasayansi siku zijazo.

96. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapandisha hadhi Shule za Sekondari za Nyamtukuza, Muhange, Shuhudia, Kasanda na Gwanumpu kuwa za Kidato cha Tano na Sita.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

97. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali inafanya juhudi gani kuboresha Mfuko wa TASAF kwa Wananchi wasiojiweza kiuchumi.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

98. MHESHIMIWA EMMANUEL LEKISHON SHANGAI (NGORONGORO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, lini Serikali itafanya tathmini ya uharibifu wa mazingira ya Mto Juhe na Mto Pinyinyi uliotokana na mafuriko – Ngorongoro.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

99. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itajenga Karakana ya Uchoraji, Ufundi Bomba, Maabara ya Kompyuta na Bweni la Wasichana katika Chuo cha VETA - Urambo.

100. MHESHIMIWA PROF. PALAMAGAMBA JOHN AIDAN MWALUKO KABUDI (KILOSA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itajenga Viwanja vya Michezo na kupeleka vifaa vya michezo katika Chuo cha Ualimu Ilonga.

WIZARA YA FEDHA:

101. MHESHIMIWA EDWARD OLELEKAITA KISAU (KITETO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, nini kauli ya Serikali katika kulinda bei ya Zao la Alizeti kwa kuongeza kodi kwenye mafuta kutoka nje ya nchi.

WIZARA YA UCHUKUZI:

102. MHESHIMIWA ALI JUMA MOHAMED (SHAURIMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, sababu gani zinasababisha Shirika la Ndege la ATCL lisitumie fursa ya kubeba Watalii wanaotoka nchi mbalimbali Duniani kuja nchini.

103. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (BLW):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, vigezo vipi vinatumika kuwatambua Wanataaluma wa Hali ya Hewa nchini kwa madaraja yao.

104. MHESHIMIWA NG'WASI DAMAS KAMANI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali haioni haja kupunguza faini za Bajaji za Mizigo kwa kukosa leseni ya usafirishaji kutoka Tsh. 250,000/= hadi Tsh. 25,000/=.

WIZARA YA UJENZI:

105. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Masasi - Nachingwea kwa kiwango cha lami hasa baada ya kusainiwa Mkatiba wa EPC +F.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**106. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA
(RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Ofisi ya Uhamiaji Rungwe itapatiwa gari kwa ajili ya kukabiliana na Wahamiaji Haramu.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

**107. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS
(KINONDONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ipi kauli ya Serikali juu ya majengo ambayo ujenzi wake umesimama kwa muda mrefu Dar es Salaam pamoja na kuweka Sheria ya ukomo wa ujenzi.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

(Majadiliano yanaendelea)

DODOMA
17 APRILI, 2024

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE

